JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA KWANZA

06 SEPTEMBA, 2016

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 06 SEPTEMBA, 2016

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 1. MHESHIMIWA AZZA HILLAL HAMAD (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini ambayo imeanzishwa kwa nguvu za Wananchi wakishirikiana na Halmashauri.

### 2. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Tangu ilivyotangazwa kuwa elimu ni bure, Walimu wengi wanaofundisha shule za awali (chekechea) wameondoka katika shule walizokuwa wanafundisha na kuanzisha vituo vyao kwa sababu ya kutolipwa:-

Je, Serikali haioni kuwa hili ni tatizo kwa wanafunzi hao ambao wanahitaji msingi mzuri;

**3. MHESHIMIWA FREEMAN AIKAELI MBOWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Ongezeko la ukubwa wa Serikali na watumishi wake linatokana na kuongezeka mara kwa mara kwa Mitaa, Vijiji, Kata, Tarafa, Majimbo ya Uchaguzi, Wilaya na Mikoa na hivyo kuongeza ukubwa wa bajeti ya Serikali kwenye mishahara, matumizi mengine (OC) na kusababisha kupungua kwa ongezeko la bajeti ya maendeleo na hata wakati mwingine upatikanaji wake:-

(a) Je, ni Vitongoji, Vijiji, Mitaa, Kata, Tarafa, Majimbo, Wilaya na Mikoa mingapi imeongezeka mwaka hadi mwaka kuanzia mwaka 2000 hadi 2015;

(b) Je, ongezeko hili limesababisha vipi ukuaji wa idadi ya watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa na mishahara imepanda vipi mwaka hadi mwaka kuanzia mwaka 2000 hadi 2015 na ongezeko hilo ni asilimia ngapi ya bajeti ya Serikali;

(c) Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu mkubwa wa kusitisha ukuaji wake ili kuelekeza fedha

zinazogharamia utawala kwenda moja kwa moja kwenye bajeti za maendeleo ya wananchi.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**4. MHESHIMIWA DANIEL EDWARD MTUKA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni imepata USD 17 milioni kutoka katika mgao wa sh. Usd 500 mil. zilizotolewa na Serikali ya India kusaidia miradi ya maji kwa bajeti ya 2016/2017:-

Je, ni lini fedha hizo zitaanza kupelekwa katika Halmashauri husika hasa ikizingatiwa kuwa shida ya maji imezidi kuwatesa wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na kwingineko katika nchi yetu kwa ujumla.

**5. MHESHIMIWA GEORGE HURUMA MKUCHIKA (NEWALA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Mradi wa maji wa Makonde ulijengwa mapema miaka ya hamsini kwa lengo la kuondoa kero ya maji katika uwanda wa Makonde wenye Wilaya za Newala, Tandahimba na sasa Mtwara Vijijini lakini mitambo ya mradi huo imechakaa sana na watumiaji wameongezeka na hivyo kufanya

upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Newala kuwa asilimia 31 tu:-

Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo na inachukua hatua gani za kulitatua.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**6. MHESHIMIWA VENANCE METHUSALAH MWAMOTO (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, kwa nini Serikali isifute michezo Tanzania.

**7. MHESHIMIWA DKT. MARY MACHUCHE MWANJELWA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- Kila jamii ina mila, desturi na tamaduni zake; hapa nchini wanamuziki wa kike wamekuwa wakivaa mavazi yasiyo ya staha na kufanya utu wa mwanamke kudhalilishwa kutokana na kuvaa nguo zinazoonyesha maungo yao:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti mavazi yasiyo na staha kwa wanamuziki wa kike.

## WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

**8. MHESHIMIWA MARWA RYOBA CHACHA (SERENGETI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Zao la Tumbaku limekuwa likilimwa sana Wilaya ya Serengeti lakini kuna changamoto kubwa ya kukosa masoko:-

Je, ni lini Serikali itasaidia upatikanaji wa Kampuni zaidi ya moja kwenye ununuzi wa tumbaku ndani ya Wilaya ya Serengeti.

## WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

**9. MHESHIMIWA SAADA MKUYA SALIM (WELEZO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Vituo vingi vya Afya vya Jeshi vinahudumia Maafisa wa Jeshi na Wananchi waliopo karibu na vituo hivyo. Hata hivyo vituo hivi vinakabiliwa na upungufu wa dawa, vifaa tiba na wataalam wenye ujuzi:-

(a) Je, Serikali inafahamu idadi ya vituo vyake vilivyopo Zanzibar;

(b) Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha kuwa vituo hivyo vinapatiwa dawa, vifaa tiba na wataalam ili kuhudumia wananchi.

**10. MHESHIMIWA RASHID MOHAMED CHUACHUA (MASASI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Kumekuwepo na malalamiko kwa upande wa huduma za afya kwa Wanajeshi wetu ambao kimsingi hawana Bima ya Afya kwa sababu Jeshi lina Zahanati na Hospitali zake:-

Je, Serikali haioni haja ya kuwapatia Wanajeshi Bima ya Afya.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**11. MHESHIMIWA JUMA KOMBO HAMAD (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kwa muda mrefu sasa kikosi cha Polisi Marine Pemba hakina boti za doria hali inayosababisha Polisi kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kila siku:-

Je, Serikali inalitambua tatizo hilo, kama inalitambua ni lini itakipatia kikosi hicho boti za

doria ili kuwawezesha Polisi hao kufanya kazi zao kwa ufanisi.

**12. MHESHIMIWA RITTA ERNESPHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

(a) Je, ni lini Askari wa Iringa watajengewa nyumba;

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha wanachodai Askari wa Mkoa wa Iringa cha posho na stahiki zao zingine.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**13. MHESHIMIWA ISSA ALI MANGUNGU (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Jimbo la Mbagala lina wakazi zaidi ya laki nane (800,000) kutokana na sensa ya watu na makazi lakini ina Mahakama ya Mwanzo Kizuiani tu:-

(a) Je, kwa nini Serikali imeshindwa kujenga Mahakama katika Jimbo la Mbagala kwa kuzingatia idadi kubwa ya wakazi;

(b) Kwa kuwa kuna mahitaji makubwa ya huduma za Mahakama Jimbo la Mbagala katika Kata za Chamazi, Mbande, Kijichi, Kibungwa, Kibondemaji na Tuangoma; Je, Serikali ipo tayari kujenga Mahakama katika Kata hizo hata kwa mpango wa dharura.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**14. MHESHIMIWA BAHATI ALI ABEID (MAHONDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Simu feki zimezimwa kwa sababu ya madhara ya kiafya kwa Watanzania:-

(a) Je, Wananchi wanaoendelea kuzitumia kwa matumizi mengine hazitawaletea madhara ya kiafya;

(b) Kama zina madhara Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kutoa elimu kwa umma.

15. **MHESHIMIWA BALOZI DKT. DIODORUS BUBERWA KAMALA (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kwa muda mrefu kumekuwepo ahadi ya kulipa fidia wananchi waliotoa maeneo yao kupisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kajunguti:-

(a) Je, ni lini wananchi wanaohusika watalipwa fidia walizoahidiwa;

(b) Je, ujenzi wa uwanja huo utaanza lini.

## III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Habari wa Mwaka 2016 *(The Access to Information Bill, 2016)*

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**06 SEPTEMBA, 2016** **KATIBU WA BUNGE**